



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



TANGAZO KWA WANASHERIA WALIOPO KWENYE UTUMISHI WA UMMA WENYE NIA YA
KUOMBA KUTEULIWA KUSHIKA NAFASI YA WAKILI WA SERIKALI WA MKOA
(EXPRESSION OF INTEREST)

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria kwa mujibu wa Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inakaribisha Wanasheria wote waliopo ndani ya Utumishi wa Umma ambao wamesajiliwa katika Daftari la Mawakili wa Serikali ambalo linasimamiwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali wenye nia ya kuteuliwa kuwa Wakili wa Serikali wa Mkoa katika mkoa wa Mara, Shinyanga, Kigoma, Singida, Katavi, Iringa, Ruvuma, Songwe na Morogoro; kuwasilisha Wasifu (CV) yake kwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

1. Sifa za Waombaji:

- Awe Mtumishi wa Umma;
- Awe na Shahada ya Uzamili ya Sheria (LL.M) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali;
- Awe amehitimu Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo (Law School) na kufuzu ipasavyo;
- Awe amesajiliwa katika Daftari la Mawakili wa Serikali na kupata namba ya usajili (State Attorney Roll Number);
- Awe Wakili wa Serikali/Afisa Sheria Mwandamizi;
- Awe na uzoefu wa kazi unaoendana na majukumu ya nafasi husika; na

2. Majukumu ya Jumla ya Nafasi:

- Mshauri Mkuu wa masuala yote ya Kisheria kwenye Mkoa husika kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- Kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi za Serikali zilizopo ndani ya mkoa husika;
- Kushughulikia malalamiko mbalimbali ya kisheria yanayowasilishwa katika Ofisi ya Mkoa;
- Kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa na kusimamia Kamati za Ushauri wa Kisheria ngazi ya Wilaya;

- Kuandaa na kuratibu Kliniki za Sheria Katika Mkoa na Wilaya zake;
- Kufuatilia utekelezaji wa mikataba katika miradi mbalimbali ndani ya mkoa husika;
- Kuwa kiungo muhimu kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kusimamia masuala ya mashauri Mahakamani;
- Kusimamia Mwakili wa Serikali kitaaluma katika Mkoa kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- Kumuita Afisa yeyote wa Serikali kutoa ufafanuzi katika masuala ya kisheria;na
- Kuandaa na kuendesha vikao vya masuala ya kitaaluma ndani ya mkoa husika.

3. Maelekezo Muhimu kwa Muombaji:

- Muombaji wanatakiwa kuhuisha (update) Wasifu wake (CV) kupitia Daftari la Mwakili wa Serikali lililopo katika mfumo wa OAG MIS kabla ya kuwasilisha maombi;
- Muombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma na cheti cha usajili wa Uwakili;
- Barua ya maombi ipitishwe na Mwajiri;
- Muombaji awasilishe maombi kupitia parua pepe: rsa.apply@oag.go.tz.
- Maombi yatakayowasilishwa ana kwa ana hayatapokelewa.
- Wenye uzoefu au makazi katika mikoa hiyo wanashauriwa kuomba;
- Muombaji awe amehuisa taarifa zake katika Mfumo wa OAG-MIS;
- Mwakili Wandamizi waliopo katika mikoa husika wanashauriwa kuomba.

4. Mwisho wa Kupokea Maombi;

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 28 Aprili, 2026 saa 09:30 Alasiri.**

Maombi yatakayowasilishwa nje ya muda hayatafanyiwa kazi.

Imetolewa na:

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI